

# MTAZAMO WA ULIMWENGU

**Kitabu cha mwongozo wa mawazo ya kibiblia na mtindo wa maisha**

NA KATHERINE GALLAGHER

# Mtazamo wa ulimwengu

## Kitabu cha mwongozo wa mawazo ya kibiblia na mtindo wa maisha

NA KATHERINE GALLAGHER

# Haki miliki

Haki miliki @ 2026 GoStrategic

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya chapisho hili inaweza kunakiliwa, kuhifadhiwa katika mfumo wa kurejesha au kusambazwa; kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile isipokuwa nukuu fupi fupi katika mapitio muhimu au Makala; bila idhini ya maandishi kutoka kwa mchapishaji.

Imechapishwa na GoStrategic

1221 Farmers Lane, Suite E Santa Rosa, CA 95405 USA
www.gostrategic.org|info@gostrategic.org

Kimeandikwa na Katherine Gallagher kutokana na mafundisho ya sauti ya Adam Peacocke, Dennis Peacocke na Katherine Gallagher

Kimehaririwa na Allison Thomson, Katelyn Mcleod na Bruce Billington

Mfasiri Msingi Pauline Auma

Mapitio ya ziada ya tafsiri na Lillian Kirui, Nigel Otieno, Simon Elia, Stanley SK Kamau na Michael Gacheru

# Utangulizi:
# Kwanini Mtazamo Wa Ulimwengu Ni Muhimu

KUSUDI LA KITABU HIKI ni kuchunguza na kuhusisha mambo ya Imani kuhusiana na Maisha yetu ya kila siku; na kuelewa jinsi mtazamo wetu wa ulimwengu unavyoathiri fikra na mtindo wetu wa maisha. Lengo letu ni wewe kupata ufahamu bora unaokusaidia kuelewa **mtazamo wa ulimwengu ni nini, na kwa sababu gani ni muhimu kuuelewa.**

Labda unafikiri “mimi si mchungaji au kiongozi wa kanisa. Sipendezwi sana na falsafa, sina nia ya kuhudhuria seminari au kusomea saikolojia. je hili linanihusu kweli?” Jibu ni “ndiyo”. Mtazamo wa ulimwengu sio

tu sehemu ya ziada ya uhusiano wetu na Mungu, ila ni sehemu kuu ya uhusiano wetu na Yesu. Ni muhimu kwa ukuaji na ukomavu wetu wa kiroho.

Wakati watu wengine hutumia neno "mtazamo wa ulimwengu" wanaelezea mafunzo yanayolinganisha dini tofauti. Tawi hili la uchunguzi linahusisha utaratibu wa kulinganisha mafundisho ya dini za ulimwengu. Ingawa ujuzi wa dini zingine ni wa thamani, hili sio lengo la mafunzo haya. Kwa madhumuni yetu, **mtazamo wa ulimwengu ni mafundisho ya kuelewa tunayoyaamini kuhusu maisha, ulimwengu na jinsi tunavyoweza kuyatekeleza.**

Maswali na mawazo yaliyowasilishwa hapa yanamhusu kila mtu! Sisi sote ni watumwa wa fikra na imani yetu, na fikra hizi zinaweza kuwa za ukweli au udanganyifu. Kile tunachohisi kama ukweli-mtazamo wetu wa

dunia- huamua kadirio na chaguo letu. Kila wazo lina matokeo yake. Mawazo haya yanaunda imani na uhakika, na kuimarisha tabia ya mtindo wa maisha yetu.

## Unaweza kuwa umeokolewa, na usiwe na mtazamo wa ulimwengu wa kikristo.

Tunapoamua kumfuata Yesu, yeye huanza kubadili mioyo yetu na kutupa utambuzi wa maamuzi yetu. Hata hivyo, fikra zetu za awali haziletwi katika upatanisho moja kwa moja na neno na tabia ya Mungu. Ni wajibu wetu kukagua mtazamo wetu wa ulimwengu na kuupatanisha na kanuni za Mungu. Hii inamaanisha kuwa unaweza kuwa umeokolewa na usiwe na mtazamo wa ulimwengu wa KiKristo.

## Mtazamo wa ulimwengu ni nini?

Mtazamo wetu wa ulimwengu ni imani ya mambo fulani ya kibinafsi [tunayodhania] tunayoshikilia kuhusu jamii, tamaduni, na ulimwengu unaotuzunguka, ambao huamua jinsi ukweli wetu utakavyokua.

Labda unafikiri, je, Mungu anajali ninachofikiria kuhusu mambo yanayoendelea? Je, kile ninachoamini kuhusu asili ya dunia au jamii kina uhusiano wowote na imani yangu na Mungu? Jibu ni ndio! Mtazamo wa ulimwengu una uhusiano mkubwa na kila jambo linalohusu maisha, na ndiyo maana ni muhimu kwa wakristo kuelewa ulimwengu kupitia mtazamo wa Mungu. **Yale tunayoyaamini, kwa kufahamu au kutofahamu yanaathiri uamuzi, mtindo wa maisha na ushawishi wetu.**

Hebu tuangalie Biblia inasemaje kuhusu kubadilisha makadirio yetu:

*Angalieni mtu yeyote asiwafanye ninyi mateka kwa elimu batili na madanganyo matupu yanayotegemea mapokeo ya wanadamu na mafundisho ya ulimwengu badala ya kristo.*

—WAKOLOSAI 2:8

*Wala msiifuatishe namna ya ulimwengu huu, bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu. Ndipo mtaweza kuonja na kuhakikisha ni nini mapenzi ya mungu yaliyo mema, yanayopendeza machoni pake na ukamilifu.*

—WARUMI 12:2

*Hubiri neno, kuwa tayari wakati ufaao na wakati usiofaa; karipia, kemea na utie moyo kwa uvumilivu wote na kwa mafundisho mazuri.kwa maana wakati utakuja watu watakapokataa kuyakubali mafundisho yenye uzima. Badala yake; ili kutimiza tamaa zao wenyewe, watajikusanyia idadi kubwa ya walimu*

*wapate kuwaambia yale ambayo masikio yao yanayowasha yanatamani kuyasikia. Watakataa kusikiliza kweli na kuzigeukia hadithi za uongo.*

—2 TIMOTHEO 4:2-4

Maandiko yamefafanua kwamba tunapaswa kulinda mioyo yetu, kuchunguza imani yetu na kuelekeza mawazo yetu ili kuhakikisha kwamba mawazo na maamuzi yetu yanaundwa na kuongozwa na Mungu pekee. Ndani yetu tunashikilia upendeleo wa kibinafsi. Katika jamii, tunatazamia wanadamu wengine wasio wakamilifu kuwa na majibu. Kutegemea mitazamo hii yenye kasoro haiwezi kamwe kuzaa haki ya Mungu.

Ukweli ni kwamba tunaweza kufahamu au kutofahamu kwa ukamilifu imani yetu yote. Tunaweza kutumia maneno kama "kufahamu na kutofahamu imani yetu" au "imani tafakari na zisizo tafakari." Kwa njia nyingine tunaweza kuwa tumechagua falsafa fulani, au

kupitisha kundi la mambo ya imani kama maslahi ya msingi, bila kujua kwamba mtazamo wetu wa ulimwengu ulikuwa ukichochewa na hali na vishawishi katika maisha yetu.

Wakristo wengi leo wana kile kinachoitwa "mtazamo wa ulimwengu uliochanganyika." Huu ni mchanganyiko wa mafundisho na imani kutoka kwa dini au falsafa nyingi. Wanampenda Yesu lakini wanashikilia imani mbalimbali kutoka kwa vyanzo vingine na kuzaa mtazamo wa ulimwengu uliochanganyika. Mtazamo huu uliochanganyika huzaa ujumbe uliochanganyika- na mara nyingi mtindo wa maisha usiomwakilisha Yesu. Ni vyema kuwa waumini walio na mtazamo sahihi wa ulimwengu wenye msingi wa kibiblia na kanuni ambazo zilihamazisha maisha ya Kristo.

Imani kwa kawaida inategemea ushahidi halisi na ukweli ulioshuhudiwa. Vivyo hivyo, imani inaweza kukita mzizi katika uamini wetu hata wakati ambapo hatuna kweli zote. Kuna kipengele cha uaminifu katika imani. Bila kujali uhusiano wa kidini, kila mtu huweka imani kwa kitu au jambo fulani.

Swali sio "je unaishi kwa imani?" bali ni "unaishi kwa imani gani?" Hatimaye, kila mtu huuliza "kwa nini niko hapa?" na kila mtu huchagua jibu la swali hilo. Kwa hivyo, kila mtu ana mtazamo wa ulimwengu-iwapo anatambua au hatambui.

**Somo hili litafafanua mtazamo wa ulimwengu katika sehemu tatu:**

- **Udhanio wetu** (kilicho ndani ya mioyo yetu)
- **Kilicho na ushahidi** (yale yaliyo kwenye akili zetu)
- **Utekelezaji** (jinsi tunavyoishi na kutenda)

## Sote tuko katika safari ya mtazamo wa ulimwengu.

Katika safari ya kugundua mtazamo wetu wa ulimwengu, tunaanza kwa kushawishiwa. Kuna nyakati ambazo tunakabiliwa na mitazamo tofauti, na ni lazima tuamue jinsi ya kujibu. Ikiwa tutachagua kulinganisha fikra zetu na neno la Mungu, tutaelekeza namna yetu ya katika kweli na kuijumuisha katika maisha yetu. Kwa hivyo, tunaanza kuishi Katika mipangilio ya kiungu na sio kwa kufikiria kwetu.

Mtazamo wa ulimwengu na kujifunza jinsi ya kufikiria [sio kile cha kufikiria] kunahitaji kuuliza maswali mengi!

**Maswali matatu muhimu huamua mtazamo wa vile mambo yalivyo, na tabia zetu:**

1. Je tunaamini nini kuhusu ASILI YA MUNGU?

2. Je tunaamini nini kuhusu ASILI YA MWANADAMU?
3. Je tunaamini nini kuhusu ASILI YA UKWELI?

**"Asili" ya kitu inaweza kuamuliwa kwa kuuliza:**

- Je, ipo?
- Je, inafanana na nini?
- Je, tunaifafanuaje?

## Mtazamo wa ulimwengu ni safari ya maisha katika ukweli.

Hakuna njia za mkato za kuboresha maisha yetu, kushugulikia hoja kwa ufanisi, na kupata mtazamo sahihi wa ulimwengu. Inahitajika kuendelea kujitolea kutengeneza njia zinazowezesha kuchunguza maamuzi, chaguo, migogoro, mahusiano na maisha yenyewe. Ingawa inachukua muda, subira na kuelewa ili kukuza aina hii ya kufikiria,

thawabu yake inafaidisha kwa maana hutupatia kiwango kikubwa cha ushawishi.

Mengi ya mazungumzo haya hutokana na uchaguzi wetu wa jinsi tunavyoishi. Je, tunafanya maamuzi gani kuhusu mambo kama dini na mtindo wa maisha? Katika tamaduni za kimagharibi, huwa tunafanya maamuzi tukitumia sheria ya, wema na ubaya ([au heshima na aibu] katika tamaduni nyingi za kimashariki). Hata hiyo, katika Bibilia, maswala haya mara nyingi huwasilishwa kama 'uhai na kifo.'

Aina moja ya mseto wa mawazo na uamuzi huleta kifo [kimwili na kiroho] na nyingine huleta uhai na uzima tele. Tunapotafuta majibu ya maswali muhimu maishani, neno la Mungu linatufundisha jinsi ya kupata uhai na uzima, wala si kifo.

> ***Leo ninaziita mbingu na nchi kama mashahidi dhidi yako kwamba nimeweka mbele yako uzima na mauti, baraka na***

*laana. Basi sasa chagueni uzima, ili wewe na watoto wako mpate kuishi.*

—KUMBUKUMBU LA TORATI 30:19

Wale ambao wameanza kuishi "kulingana na taratibu za kiungu" hugundua fursa za kukua na kushawishi wale walio karibu nao kwa ufahamu na kutofahamu. Vita huanzia mioyoni mwetu. Mioyo yetu huamua tunataka kuwa watu wa aina gani, na tuko tayari kufikia kiwango gani ili kuwa waaminifu kwa imani tunazo shikilia. Daima tutakabiliana na chaguo la vile tunavyojihusisha na watu ambao wanawasilisha mtazamo wao wa ulimwengu kwetu, au kuuliza maswali kuhusu imani yetu.

Kama wakristo, tunaweza kufanya uinjilisti tukiwa na nia ya kuwashawishi wengine kuhusu maoni yetu. Hii mara nyingi husababisha mijadala na hata mabishano kuhusu maswala makuu, huku pande zote mbili zikijaribu kuthibitisha hoja zao. Njia hii

inahatarisha kabisa kutoelewa chanzo cha mawazo ya mtu. Uinjilisti ulio mkamilifu unaoshirikisha tamaduni unahusisha kuuliza maswali sahihi- yanayosaidia watu kutambua imani zao za kimsingi-na kumruhusu Roho Mtakatifu kuwahudumia katika mazungumzo. Ni lazima tuwe tayari kuwajibika kwa imani yetu ili tusikwame katika mabishano.

**Chochote unachoweza kushawishiwa uingie, unaweza kushawishiwa utoke.**

Hatimaye, ukweli lazima uelezewe na upokelewe kwa kiwango cha moyo, na wala si kichwani tu. Tunaweza kujikuta katika mijadala inayohusu matunda na kusahau mizizi kabisa. Mara tu tunapoona na kufafanua mizizi, tunaweza kuuliza maswali sahihi. Kisha tunahitaji kuruhusu maswali hayo magumu kuzama ndani ya mtu huyo, ili kumpa nafasi ya kushindana na maswali hayo, na kumpa Mungu nafasi ya kuwavuta kwake.

Tunapoanza safari hii ya fikra za kina kupitia mtazamo wa ulimwengu, lengo letu la kwanza linapaswa kuwa juu ya kile ambacho Mungu anataka kufanya ndani yetu na kupitia kwetu. Tunapokua katika ujuzi na ufahamu, ni lazima tukumbuke kuruhusu mioyo yetu kuwa wazi mbele za Bwana. Mengine yote yatafuata.

## MUKHTASARI

- Mtazamo wa ulimwengu ni fungu la imani ya kibinafsi kuhusu utamaduni na ulimwengu unaotuzunguka.
- Mtu anaweza kuwa mkristo bila kuwa na mtazamo wa ulimwengu ulio wa KiKristo.
- Kila mtu ana mtazamo wa ulimwengu iwapo anatambua au la.
- Mtazamo wa ulimwengu ni mchakato wa maoni. Mtu ambaye ameshawishiwa kuingia katika jambo

fulani anaweza kushawishiwa kutoka kwa jambo hilo. Ni lazima tuchunguze na kuamua mtazamo wetu wa ulimwengu.

## MASWALI YA KUJADILIANA

1. Je, mtazamo wako wa ulimwengu kwa sasa umeathiriwa kwa ufahamu au kwa kutofahamu?
2. Ni njia gani rahisi ya kumuelezea rafiki dhana ya mtazamo wa ulimwengu uliyo sahihi?
3. Je, tunawezaje kulinganisha mtazamo wetu wa ulimwengu na dhamira ya Mungu?

HAKUNA MAFUNZO YA SAUTI/PICHA

# SEHEMU YA KWANZA



# Sura ya 1: Dhanio la Mtazamo wa Ulimwengu, Sehemu ya Kwanza

## Dhanio ni nini, na kwa nini ni muhimu?

KILA MTU ANA MTAZAMO WAKE WA ULIMWENGU ambao umehusisha taratibu za kimsingi zinazoitwa **dhana**. Taratibu hizo zipo iwapo mtu anazifahamu au la. Lengo letu ni kutoa ufahamu unaosaidia kuelewa dhanio ni nini, na kwa nini inaathiri imani yetu na ufahamu wa mtazamo wa ulimwengu.

Sote tuko kwenye safari ya mtazamo wa ulimwengu na huwa tunaanza kwa kushawishiwa na mambo mengi kama vile familia, utamaduni, mambo ambayo

tumekumbana nayo, utu na vipengele vingine vya mazingira. Mtazamo wetu wa ulimwengu umejengewa juu ya msingi wa kudhania. Kwa sababu mambo haya ya kudhania yaliyofichika yanaathiri maisha yetu kwa kiwango kikubwa, basi huamua kiwango cha ushawishi wa vitu vingine maishani mwetu.

> **Dhanio ni**
> *mambo yasiyo na uhakika, ambayo yanaunda mtazamo wetu wa ulimwengu; wazo, kwa ufahamu au kutofahamu, lililofafanuliwa au lisilofafanuliwa; jambo lililodhaniwa kabla ya mwanzo wa hoja, au hatua ya uamuzi*

Mtazamo wa ulimwengu wa kudhania hauhusu dini za kulinganisha, falsafa au kushinda hoja, mbali unahusu kuimarisha imani yetu. Tunapoanza safari pamoja na Mungu, na kutambua kuwa imani yetu ya kikristo inahusisha kila eneo la maisha, tunapata majibu ya maswali yote makubwa

au madogo. Tutaweza kushughulikia maswali ambayo hatujawahi kuulizwa hapo awali, au kufikiria, au ambayo hayajajibiwa kwa njia maalum kwenye maandiko.

**"Sio kuambiwa nini cha kufikiria, ila kufundishwa jinsi ya kufikiria."**

—ADAM PEACOCKE

## Kila mtu anaishi kwa imani fulani-iliyowekwa tofauti.

> *Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Maana kwa hiyo wazee wetu walishuhudiwa . . . Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wamtafutao.*
>
> —WAEBRANIA 11:1-2, 6

Imani katika Mungu ni hatua ya kwanza katika uhusiano naye. Pasipo imani, haiwezekani

kumpendeza Mungu. Safari ya imani ni kuamini kwamba Mungu yupo, na ni mlipaji wa thawabu kwa wale wanaomtafuta.

Katika kila eneo ambalo imani inahusika, tunatafuta kitu ambacho kitatuletea thawabu au hisia za thamani. Imani sio kitu kilichotulia; ni uhusiano unaohusisha kutafuta na kuendelea kukua. Je, tumeweka imani yetu kwa nani au nini? Jibu sio lazima liwe la kipekee, bali linaweza kuwa mchanganyiko wa vitu kadhaa vinavyothaminiwa kwa viwango tofauti. Kwa njia nyingine, ni sauti gani ambayo unaisikiliza zaidi?

Sote tuna ‘jopo la wataalam’ wanaochangia mawazo yetu, kushawishi imani zetu na kutengeneza maamuzi yetu. Je, ni nani aliye nyuma ya sauti zinazozungumza katika maisha yako na namna yako ya kufikiria?

## Maeneo matano ya kawaida tunayoegemeza imani yetu:

1. **Wataalamu** *(wanasiasa, wachungaji, wanasayansi na kadhalika)*
2. **Uzoefu na hisia** *(mambo ambayo yametendeka kwetu, au mambo tunayofikiri kuwa tunaelewa kutokana na matukio hayo)*
3. **Sayansi na ubunifu**
4. **Mila** *(familia, tamaduni)*
5. **Ufunuo** *(Mungu, neno)*

## MUKHTASARI

- Kila mmoja ana mtazamo wa ulimwengu, unaojumuisha mambo ya kimsingi yanayojulikana kama udhanio.
- Sio kuambiwa la kufikiria, mbali kufundisha namna ya kufikiri.
- Sote tuna 'jopo la wataalam' tunalotazamia kupata ufahamu na mwelekeo.

## MASWALI YA KUJADILIANA

1. Je, unaweza kutoa mfano wa njia rahisi ya kuelezea neno “udhanio” kwa rafiki?
2. “Jopo lako la wataalam” ni akina nani? Je, ni nani au nini unayotegemea au kuruhusu kukushawishi zaidi?
3. Ni nini cha muhimu kwa wataalamu wako katika maisha yako?

INAKUBALIANA NA KANDA YA SAUTI/ YA PICHA #1